# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA

ISSN 0856 - 1214 ■ TOLEO 01 ■ JANUARI 2021 ■ TSH. 1000/=


# Viongozi wa Dini wajadili afya, ukatili wa kijinsia

UK. 8





UK. 2

*Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Fredrick O. Shoo awaomba Wakristo kuchangia Seminari ya Kilutheri.*



UK. 17

*Historia ya Marehemu Seth Ndesanjo Kitange.*



UK. 19

*Askofu Mlezi wa vijana KKKT Dkt. Emmanuel Makala awaomba vijana kutekeleza makubalino ya Mkutano Mkuu wa nne.*



UK. 6

*KKKT na Serikali wajadili mpango kabambe wa Tiba Shufaa.*

# Michango, Seminari ndogo ya Kilutheri Morogoro



*Mkuu wa KKKT, Mhe. Askofu Dkt. Fredrick O. Shoo akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya wanakamati wa shule ndogo ya kilutheri ya morogoro na wafanyakazi wa ofisi kuu ya KKKT mara baada ya kumaliza ibada iliyoambatana na uzinduzi katika usharika wa Moshi mjini.*

Katika kuhakikisha shule ya seminari ya kilutheri iliyopo Morogoro inaendelea kujenga vijana wazuri ambao watakuwa msaada katika Taifa la Tanzania, muunganiko wa watu mbalimbali waliowahi kusoma shule hiyo ya seminari wamejitokeza na kuweka wazi nia ya wao kuichangia shule hiyo na kuomba wengine kufanya hivyo ili kuiwezesha shule hiyo kuendelea kutoa elimu bora kwa vijana nchini.

Mkuu wa Kanisa la KKKT, Mhe. Askofu Dkt. Fredrick Shoo alihudhuria na kuzindua zoezi la uchangiaji wa shule ya seminari ya kilutheri ya Morogoro, ambapo kila mkristo ameombwa kuchangia shilingi 1000, michango itakayosaidia kurekebisha majengo na miundo mbinu ya seminari hiyo ya kilutheri pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zilizopo kwenye kituo hicho cha umoja.

Akizungumza katika ibada iliyofanyika Usharika wa Moshi mjini iliyoongozwa na Mchungaji Jane Manase na mahubiri yaliyotolewa na Mchungaji Leons Shirima, Askofu Dkt. Shoo amesema kuwa shule hiyo imetengeneza vijana wazuri ambao wamekuwa msaada katika jamii zinazowazunguka kutokana na misingi mizuri waliojengewa katika shule hiyo ambalo ni jambo la kumshukuru Mungu.

Aidha Dkt. Shoo amewaomba wakristo na watu wote kuchangia kwa moyo shule hiyo kwani ni shule yao na imekuwepo kwa muda mrefu hivyo kwa kuichangia kutasidia katika ukarabati na kuifanya shule hiyo kuendelea kutengeneza vijana wazuri watakaokuwa na mchango mkubwa katika jamii zinazowazunguka.

Akiwatambulisha wanakamati wakati wa Ibada Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa amesema kuwa kamati hiyo itashughulika na michango yote ambayo itaingia benki na kutengeneza kanzi data (Database).

Baada ya kukaribishwa ili kuzungumza kwa niaba ya kamati ya waliowahi kusoma katika shule hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Dkt. Anna Mgwira, ambaye pia ni mmoja wa wanafunzi walisoma katika shule hiyo ya seminari, amesema kuwa ni vema shule hiyo ikachangiwa ili kuiwezesha kufanya vizuri hasa katika kutoa elimu na kuwajengea vijana nidhamu na umoja.

Mkuu wa Mkoa huyo Dkt. Anna amesema shule hiyo imetoa watu wengi na miongoni mwao ni watu wenye nyadhifa kubwa wanaofanya kazi

Inaendelea Uk. 6



*Baadhi ya wanakamati ambao pia waliwahi kusoma Shule ya Seminari ndogo ya Kilutheri Morogoro wakifuatilia Ibada ya Uzinduzi wa kuichangia shule hiyo.*

**Uhuru na Amani**
Gazeti la KKKT
**Toleo la 1, 2020**

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano KKKT.

Maoni yaliyoko katika makala zilizochapishwa ni mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya kanisa wala Mhariri, isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi. Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

Mhariri
Uhuru na Amani
S. L. P. 3033
Arusha

Barua pepe: erickin@elct.or.tz
Simu: +255-769-637-565
Tovuti: http://www.elct.org

Mhariri
ERICK K. ADOLPH

WACHANGIAJI WA MAKALA

Joram Nkya
Peter Kayombo

Limepigwa Chapa na:
Moshi Lutheran Printing Press
S. L. P. 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

## Maoni ya Mhariri

# Amani

Amani na Upendo ndio jambo tunalojivunia watanzania Duniani kote. Amani hii ndio inayotufanya watanzania wa Itikadi mbalimbali na Kabila zaidi ya 120 kuishi pamoja bila ya kuwa na vurugu.

Amani iliyopo Tanzania ni msingi wetu uliowekwa na Mungu, hivyo kutunza na kuiendeleza ni jukumu letu ili tuweze kuwa na maendeleo kuanzia ngazi ya mtu binafsi na Taifa kwa ujumla.

Amani inapaswa kuendelea kutunzwa wakati wote ili kuhakikisha kuwa haipotei katika mazingira yoyote yale.

Amani na upendo bila kujali tofauti za kidini, kikabila, rangi, elimu, uchumi n.k ndio itakayozidi kutuvusha na kuendelea kuwa na mafanikio yaletayo maendeleo chanya katika jamii ya watanzania.

Kupoteza Amani ya nchi ni sawa na kupoteza kitu chenye thamani kubwa na ipo gharama kubwa itayowagharimu watu kuitafuta na kuijenga tena Amani ambayo kuibomoa huwa ni rahisi lakini kujenga huhitaji muda na uvumilivu mkubwa.

Inapaswa kuendelea kujifunza kwa wenzetu ambao mwanzoni walikuwa na Amani lakini hivi sasa maisha yao hayana matumaini ya baadae mara baada ya kukosa tumaini katika kuiona siku inayofuata.

Yapo mataifa ambayo kwa sasa wapo kwenye migogoro mikubwa kwasababu ya kupoteza Amani kitu ambacho kimewagharimu wao na vizazi vyao kwa muda miaka mingi.

Kulijenga taifa lenye mshikamano, upendo na Amani si kitu rahisi, yapo mataifa kwa sasa yanahangaika kurejesha Amani katika nchi zao lakini bado kazi hiyo haijawa rahisi na imechukua muda mrefu kupata suluhu.

Hatuna budi kama wakristo na watanzania wote kwa ujumla kumshukuru Mungu juu ya Amani tuliyonayo na zaidi kuendelea kuomba ili Amani yetu idumu Daima.

# Maandalizi ya Kitabu cha Nyumba Kwa Nyumba 2021 yakamilika

**Kitabu cha nyumba kwa nyumba hutoka kila mwaka, na zaidi ya nakala 50,000 husambazwa kwenye Dayosisi zote za KKKT.**



*Baadhi ya wanakamati wa kitabu cha nyumba kwa nyumba wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza maandalizi ya kitabu hicho.*

Maandalizi ya awali ya kitabu cha Nyumba kwa Nyumba ambacho huandaliwa chini ya Idara Misioni na Uinjilisti inayoongozwa na Naibu Katibu Mkuu KKKT, Mch. Lazaro Rohho yamekamilika na hivyo kusubiri hatua ya mwisho iliyobaki ili kitabu hicho kiweze kusambazwa kwenye Dayosisi zote za KKKT.

Katika maandalizi ya kitabu hicho, kamati yenye wajumbe 7 hukutana kila mwaka katika zoezi la kuandaa kitabu hicho ambapo huwa msaada kwa wakristo nchini kuweza kujifunza kwa undani masomo mbalimbali yaliyopo katika Biblia ambayo ndiyo mwongozo wa wakristo wote Duniani.

Kamati ya nyumba kwa nyumba hufanya maandalizi ya kitabu hicho kwa muda wa takribani wiki moja. Wanakamati hupata muda mzuri wa kuchambua mada mbalimbali walizozitoa kwa baadhi ya watu wenye ujuzi wa aina tofauti tofauti kama vile masuala ya kiimani, uchumi, malezi, vijana na nyingine nyingi kabla ya kuingiza katika kitabu hicho.

"Kitabu cha nyumba kwa nyumba kimejaa mafundisho mazuri yaliyojikita katika Nyanja mbalimbali za kimaisha kama vile imani, uchumi, mafundisho kwa vijana na mengine mengi mazuri ikiwa na lengo la kuwajenga wakristo kiroho na kimwili."

Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti Mch. Rohho amesema kuwa katika maandalizi ya kitabu hicho huzingatia mada tofauti tofauti na hasa baadhi ya mada zile zinazowasumbua watu katika maisha yao ya kawaida kisha wao huzifafanua na kuzielezea ili kuwaongezea watu uelewa wa mambo ambayo kwao huwa ni changamoto.

> "Kitabu cha nyumba kwa nyumba kimejaa mafundisho mazuri yaliyojikita katika Nyanja mbalimbali za kimaisha kama vile imani, uchumi, mafundisho kwa vijana na mengine mengi mazuri ikiwa ni lengo la kuwajenga wakristo kiroho na kimwili."

Kitabu hicho cha nyumba kwa nyumba huwa kinatoa nafasi ya watu kujadili mada ya siku na watu wanapata muda mzuri kuweza kubadilishana mawazo wakati wanapofanya ibada za nyumba kwa nyumba na pale changamoto zinapotokea kwenye mada fulani basi kitabu huelekeza wanajumuiya kumwona Mchungaji wao ili awasaidie katika mada hiyo ama kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na Idara ya Misioni na Uinjilisti ya KKKT.

Kitabu cha nyumba kwa nyumba hutoka kila mwaka, na zaidi ya nakala 50,000 husambazwa kwenye Dayosisi zote za KKKT.



*Baadhi ya wanakamati wa Kitabu cha Nyumba kwa Nyumba wakijadili jambo wakati wa maandalizi ya Kitabu hicho.*

# Vijana KKKT wakutana Mtandaoni kujadili rushwa na madeni

Mratibu wa Vijana KKKT, Mch. Frank Mng'ong'o, hivi karibuni amefanya mkutano na vijana wa KKKT kwa njia ya mtandao wakijadili kuhusu mada ya Rushwa na Madeni Barani Afrika.

Mkutano huo uliowakutanisha vijana zaidi ya 26 kutoka Dayosisi za KKKT, ulianza kwa kumkaribisha Mhe. Askofu Dkt. Emmanuel Makala ambaye ni Askofu Mshauri wa Vijana KKKT, na kuwakaribisha pia Mchungaji Anza Lema (Mratibu wa vijana KKKT aliyemaliza kipindi chake) pamoja na Mchungaji Anicet Maganya ambaye ni Mratibu wa Ofisi ya Mkuu wa Kanisa.

Katika ufunguzi wa Mkutano huo Mchungaji Anicet Maganya alianza kwa kusoma neno la Mungu, Kutoka 23:8 na Mika 6:8.

Mchungaji Maganya alisisitiza kuhusu ubaya wa rushwa na madhara yake kwa mtu, ambapo hupelekea kuwafumba macho watoa haki mara baada ya kupokea rushwa.

Mchungaji Manganya aliwaasa vijana kuepukana na rushwa pamoja na mazingira chochezi ya kutoa au kupokea rushwa.

Aidha, Mhe. Askofu Dkt. Makala alisisitiza kuhusu uadilifu ambapo ukizingatiwa huweza kuondoa suala la rushwa katika maisha ya watu.

"Chanzo kimojawapo cha rushwa ni kukosa udilifu, hivyo ni vyema vijana wakatambua hilo na kulifanyia kazi" alisema Askofu Dkt. Makala

Mhe. Askofu Dkt. Makala ameongeza kuwa watu wameacha maongozi ya kidini na hivyo wamekosa hofu ya Mungu ndani yao na hiyo husababisha mianya ya rushwa kujitokeza ndani ya Jamii.


Ameongeza kwa kusema kuwa, mipango na mikakati mingi kwa sasa isiwekwe kwenye kupambana na rushwa maana haitosaidia sana bali ni vema kuwekeza kwa watu katika kuwajengea maadili ili waweze kuyafuata na hivyo itasaidia katika kupunguza na kuondokana kabisa na tatizo la rushwa.

Wakati wa uwasilishaji wa mada katika mkutano huo, Bi. Regina Fredrick kutoka Dayosisi Kusini Mashariki ziwa Victoria ambaye aliwasilisha mada kuhusu madeni Barani Afika na hasa deni la Taifa (Tanzania) alisema kuwa changamoto na tatizo kubwa kwa nchi nyingi za Afrika ni kuwa na bajeti kubwa kuliko kiasi ambacho wanaweza kutengeneza kwa kukusanya mapato na hivyo huwalazimu kukopa na kuziingiza nchi zao kwenye madeni makubwa.

"Taarifa za mikopo ziwe wazi na hii itasaidia watu kujua nini kinaendelea, pia Bunge liwe imara kusimamia mikataba ya mikopo ili kuondokana na madeni yasiyo ya lazima" alisema Regina Fredrick.

Rizikiael Kileo Kutoka

Inaendelea Uk. 8




*Mratibu wa Vijana KKKT, Mch. Frank Mng'ong'o akiratibisha mkutano kwa njia ya mtandao katika Ofisi Kuu ya KKKT Arusha hivi karibuni.*



*Regina Fredrick mmoja wa wasilisha mada katika mkutano uliendeshwa kwa njia ya mtandao hivi karibu.*



*Rizikiael Kileo mmoja wa wasilisha mada katika kikao kilichofanyika kwa njia ya mtandao.*



*Vijana mtandaoni.*

# KKKT, Serikali zajadili tiba shufaa



*Mkurugenzi wa Afya KKKT Dkt. Paul Mmbando (aliyekaa katikati) akiwa na wafanyakazi wa Serikali wakijadili Mpango kabambe wa Tiba Shufaa utakaotekelezwa na KKKT na Serikali.*

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania limekuwa likitoa huduma za afya ya Tiba shufaa kwa muda wa zaidi ya miaka 20 hasa ikiwa ni katika kuunga mkono juhudi za Serikali na pia kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ili kuweza kuwasadia katika kutatua changamoto mbalimbali za afya nchini.

Programu ya Afya na Diakonia KKKT imekuwa ikiratibisha shughuli zote za afya ndani ya Kanisa ambapo hivi karibuni imeshirikiana na Serikali katika kujadili muungozo mpya wa mpango kabambe wa afya ili kujumuisha huduma za tiba shufaa katika mipango ya vituo vya huduma za afya ngazi ya hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati.

Muongozo huo wa mpango kabambe unajumuisha mipango yote ya utoaji huduma za afya kwa ngazi ya zahanati na ngazi za Halmashauri.

Programu ya Afya na Diakonia KKKT inayoongozwa na Mkurugenzi wa Afya KKKT, Dkt. Paul Mmbando imekuwa mstari wa mbele katika kuisaidia jamii nchini na kwa sasa Kanisa lina vituo vya huduma takribani 30 ambavyo hutoa huduma ya tiba shufaa kwa watu zaidi ya elfu 55 kwa mwaka Tanzania Bara na Visiwani.

KKKT kama mdau mwandalizi katika kujadili mwongozo wa mpango kabambe wa afya unaojumuisha huduma za tiba shufaa katika mipango ya vituo vya huduma za afya ngazi ya hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati itaendelea kushirikiana na Serikali katika kuendelea kutoa huduma hiyo kwa ufanisi mkubwa ili kuisaidia jamii.

Dkt. Sijenunu Aron ambaye ni Mratibu wa huduma za afya Wilaya ngazi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, amesema kuwa kutokana na ongezeko la wagonjwa wanaohitaji tiba shufaa, Serikali kupitia wadau mbalimbali wa afya imeanza kuweka mipango mikakati ambayo itawezesha upatikanaji rahisi wa huduma za tiba shufaa kwa wananchi.

Kupitia Idara ya Afya, KKKT itaendelea kuboresha huduma za afya nchini kwa kuboresha huduma hizo katika vituo mbalimbali na pia kwa kuwasogezea jamii huduma za afya karibu nao ili kuwapa urahisi wa kuzifikia huduma hizo.

> "...kutokana na ongezeko la wagonjwa wanaohitaji tiba shufaa, Serikali kupitia wadau mbalimbali wa afya imeanza kuweka mipango mikakati ambayo itawezesha upatikanaji rahisi wa huduma za tiba shufaa kwa wananchi.

# Michango Seminari

Inatoka Uk. 2

ndani na nje ya nchini.

"shule hii imetoa watu wengi, wapo wafanyabiashara wakubwa, wapo wanaofanya kazi wizarani, viongozi wa kisiasa, wakurugenzi watangazaji, waalimu, majaji sita na wengine wengi" amesema Dkt. Anna Mgwira.

Mkuu wa Mkoa huyo ametoa wito kwa Dayosisi zote kuendelea kuungana na kufanya kazi za umoja ili kuendelea kulijenga Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Mkuu wa Kanisa Dkt. Shoo akihitimisha zoezi hilo katika ibada, amewashukuru na kuwatakia Baraka za Bwana watu wote watakao shiriki katika zoezi hilo na kutoa rai kwa wanakamati kufanya kazi hiyo kwa bidii, uwazi na kwa kutoa taarifa ya jinsi shughuli za uchangishaji zitakavyokuwa zinaendelea.

# KKKT yaadhimisha wiki ya watu wenye ulemavu

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania limekuwa likitekeleza Programu ya Maisha Endelevu na Uwezeshaji tangu mwaka 2011 iliponzishwa rasmi.

Lengo kuu la Programu ni kuwawezesha wanajamii wote katika maeneo mbalimbali Nchini. Kupitia Programu hii Kanisa linajenga uwezo wa kukuza uchumi kwa kaya zenye kipato duni, kuziwezesha kuwa na uhakika wa chakula (food security), utunzaji wa mazingira na kuwajengea uwezo wanajamii, viongozi wa dini na Serikali katika ngazi za vijiji na kata kwa kuzingatia Haki za binadamu kwa maendeleo. Mkazo ukiwa katika Haki za kijinsia kwa wanawake na wanaume na elimu kwa watoto.

Mradi huu wenye lengo la kuwawezesha watu wenye uziwi kufikiwa na Habari Njema za ufalme wa Mungu kwa njia ya kuanzisha Huduma ya Lugha ya Alama na Ukalimani wakati wa Ibada katika sharika za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Malengo mengine madogo ni pamoja na kuanzisha na kuhakikisha huduma ya Ukalimani katika hospitali na vituo vya afya vya Kanisa inapatikana ili wakati wote viziwi waweze kupata huduma za afya kwa usahihi na kwa wakati.

Jukumu kubwa la Mradi huo ni kutoa mafunzo ya Lugha ya Alama na Ukalimani kwa watumishi wa Kanisa kutoka katika sharika, mashule, hospitali na vituo vya afya n.k.

Mafunzo hayo hutolewa kwa muda wa miezi sita na mpaka sasa watumishi wa Kanisa 49 wamepatiwa mafunzo hayo na wanaendelea kutoa huduma ya ukalimani katika maeneo yao husika.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania lilipata nafasi ya kushiriki wiki ya maadhimisho ya Viziwi Kimataifa kupitia Dayosisi ya Mashariki na Pwani



*walemavu wa kutokusikia wakiimba kwa kutumia lugha ya Alama wakati wa Ibada ya Maadhimisho ya viziwi iliyofanyika katika Usharika wa Salasala DMP.*

katika Usharika wa Salasala.

Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) ni kati ya Dayosisi za KKKT ambazo zilizotuma watumishi wake kujifunza Lugha ya Alama. Mpaka sasa jumla ya watumishi 10 kutoka Dayosisi ya Mashariki na Pwani wamekwishapatiwa mafunzo ya Lugha ya Alama na Ukalimani.

Zaidi sana Dayosisi imeanzisha huduma ya Ukalimani kwa watu wenye ulemavu wa uziwi katika sharika tatu ambazo ni Manzese, Yombo na Mji Mwema ambapo kila jumapili wastani Viziwi 67 wanapata nafasi ya kumwabudu Mungu pamoja na washarika wengine.

Kanisa kupitia Programu ya



*walemavu wa kutokusikia (waliovaa tisheti) wakifurahia jambo mara baada ya kumalizika kwa Ibada ya viziwi katika Usharika wa Salasala DMP.*

Maisha Endelevu na Uwezeshaji linasisitiza kuwa huduma ya Ukalimali kwa watu wenye ulemavu wa kutokusikia liwe ni jambo la kuigwa na vyombo vyote vinavyotoa huduma katika Kanisa na jamii kwa ujumla.

Katika Wiki hiyo muhimu, Kanisa liliungana na watu wote Ulimwenguni kuadhimisha kwa njia ya kushiriki ibada ya pamoja katika usharika wa Salasala,

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania linatazamia kutumia sharika zinatozoa huduma ya Lugha ya Alama na Ukalimani katika ibada sio tu kuwafikishia Habari Njema watu wote kwa maana ya Misioni na Uinjilisti jumuishi bali pia kama senta au vituo vya kuwajengea uwezo watu wenye kipato duni pasipo kubagua dini, jinsi, kabila, rangi wala eneo.

Na kuhakikisha wanakuwa na uhakika na usalama wa chakula na pia kuwa sehemu muhimu kwa watu wenye ulemavu na makundi mengine mengi yanayobaguliwa, kunyanyaswa na kukandamizwa katika kaya na jamii hii ni pamoja na wanawake, watoto, vijana na wanaume ili kufika Maisha enedelevu yenye Upendo, Furaha na Amani waliobarikiwa kiroho na kimwili na wenye matumaini ya Kuurithi uzima wa milele katika Yesu Kristo.

# Vijana KKKT wakutana Mtandaoni

Inatoka Uk. 5

Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) ambaye alijikita zaidi katika kuelezea mada iliyohusu masuala ya rushwa, amesema kuwa matumizi mabaya ya nafasi ambazo watu hupewa kwa kuchaguliwa au kuteuliwa huwa ni sababu kubwa ya kuwepo kwa rushwa.

Baadhi ya vijana walipata nafasi ya kuchangia mada hizo na kuelezea mawazo yao kuwa ni namna gani Taifa likaondokana na matatizo hayo ya Rushwa na Madeni.

"Ili kuweza kupambana na matatizo ya rushwa na hasa ili vijana wasijiingize kwenye masuala hayo ni vema ikawepo miradi ambayo itawainua vijana kujikwamua kiuchumi" Alisema Naza Msangi.

Eunice George mmoja wa vijana washiriki katika mkutano huo uliwafanyika kwa njia mtandao amesema kuwa tamaa ni jambo ambalo huwagharimu sana vijana hasa katika kutaka mambo mazuri kwa muda mfupi.

"Vijana waache tama ambazo gharama zake huwa ni kubwa na huchangia sana katika kuharibu mifumo ya maisha yao" Alisema Eunice George.

Katika kuhitimisha kikao hicho cha mtandaoni Askofu Mshauri wa Vijana wa KKKT, Dkt. Emmanuel Makala aliwashukuru sana vijana kwa kushiriki na kuchangia katika mkutano huo na aliwatakia pia Baraka za Bwana ziambatane nao.

Wakati huo huo Mratibu wa Vijana KKKT, Mch. Frank Mng'ong'o aliwashukuru na kuwataka vijana kuyatendea kazi kwa nafasi zao kwa yale yaliyojadiliwa katika mkutano huo. Pia aliwataka vijana hao kuwa na utayari tena kwa kuwa maandalizi ya kikao kingine cha mtandaoni yanafanyika na watapewa taarifa mara maandalizi hayo yatakapo kamilika.

# Matendo ya ukatili kupungua



*Dkt. John Hilary, Mtathimini wa mradi wa uminywaji wa Haki na Ukatili kijinsia (aliyesimama) akiwasilisha ripoti katika Ofisi Kuu ya KKKT.*

Elimu dhidi ya matendo ya ukatili na haki za kijinsia kwenye jamii imendelea kutolewa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na hivyo kusaidia kupungua kwa matendo hayo kwenye jamii.

Katika mradi uliofanywa na KKKT na kusimamiwa na Mratibu wa Dawati la utetezi wa KKKT, Bi. Besetina Joseph Saikong' ambao uliopita katika Dayosisi nne za KKKT ambazo ni Dayosisi ya Mbulu, Dayosisi ya Kati, Dayosisi ya Kaskazini na Dayosisi ya Kaskazini Kati, umeonyesha kuwa uminywaji wa haki za kijinsia na matendo ya ukatili kwenye jamii umeweza kupungua kwa takribani asilimia 60.

Mradi huo wa utawala bora na haki za jinsia unaotekelezwa na KKKT umelenga kuhakisha kuwa matendo ya ukatili katika jamii yanapungua kama sio kuisha kabisa, hivyo elimu utolewa ili kuisaidia jamii kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2018 ukiwa mradi wa miaka mitatu, na utaendelea hadi mwaka 2021 lengo likiwa kutoa msaada wa kisheria kwa jamii, na kupinga ukatili wa kijinsia.

Mratibu wa Dawati la utetezi Bi. Besetina amesema kuwa jamii inayoishi kwa Amani ndio jamii ambayo maendeleo ni rahisi kuwepo tofauti na hilo jamii iliyojaa unyanyasaji na ukatili ni vigumu kwa maendeleo kuwepo kwasababu ya kuishi kwa woga na hofu hufunya watu kushindwa kazi zao kama vile zinavyotakiwa katika suala zima la kimaendeleo.

> Mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2018 ukiwa mradi wa miaka mitatu, na utaendelea hadi mwaka 2021 lengo likiwa kutoa msaada wa kisheria kwa jamii, na kupinga ukatili wa kijinsia.



*Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (wa nne kutoka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya watenda kazi wa Ofisi Kuu ya KKKT mara baada ya kupokea tathimini ya ripoti kuhusu ukatili wa kijinsia.*

# Kalenda mwaka 2021 yakamilika



*Kamati ya Kalenda KKKT ikijadili jambo wakati wa maandalizi ya kalenda ya mwaka 2021.*

> "Nia mojawapo ya kuwepo kwa kalenda hizi ni kuhakikisha kuwa wakristo wanajifunza kila siku Neno la Mungu ili wakue Kiroho na wafanikiwe katika maisha yao"

Kamati ya Kalenda ya KKKT huwa na kazi kubwa ya kuandaa kalenda hiyo kila mwaka ambapo kwa sasa kalenda ya mwaka 2021 kwa kufuata taratibu zote imekamilika na ipo tayari kusambazwa kwenye Dayosisi zote za KKKT.

Kamati hiyo inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Askofu Charles Mjema (Askofu Dayosisi ya Pare) ambayo hukutana kila mwaka na kufanya maandalizi ya kalenda ya mwaka husika kwa kuzingatia majira ya mwaka wa Kanisa, kwa mwaka huu imekutana mjini Arusha na kufanya maandalizi ya kalenda hiyo itakayotumika mwaka 2021.

Kamati hiyo ilikaa kwa muda wa wiki mbili jijini Arusha kuanzia tarehe 27Julai–1Agosti 2020, na 29 Septemba–2 Oktoba, 2020 ikiwa na wajumbe 9 kutoka Dayosisi za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania ambao walifanya mapitio na kuandaa kalenda ya mwaka 2021.

Kalenda hiyo ambayo huandaliwa kila mwaka imekuwa na umuhimu mkubwa kwa Kanisa ambapo Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti, Mchungaji Lazaro Rohho, amesema kuwa kalenda hiyo hutoa miongozo ya masomo ya kila Jumapili na pia hutoa neno la kila siku katika wiki ambapo huwasaidia wakristo kukua kiroho na kiimani katika hali ya kumjua Mungu wanae–mwabudu.

"Nia mojawapo ya kuwepo kwa kalenda hizi ni kuhakikisha kuwa wakristo wanajifunza kila siku Neno la Mungu ili wakue Kiroho na wafanikiwe katika maisha yao" amesema Mchungaji Rohho.

Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti, Mchungaji Rohho ameongeza kuwa kupitia kalenda ya Kanisa vilevile husaidia mtu kujifunza na kuelewa Neno la Mungu kwa urahisi kwa kuwa mara nyingi watu hushindwa kusoma Biblia kwa kuona ni kubwa au kwa kutojua ni mahali gani asome kwa kipindi ambacho yupo na Biblia karibu, hivyo kupitia kalenda hizo za Kanisa humsaidia mtu husika kujua Neno la wakati lililo katika majira ya mwaka wa Kanisa na kuweza kujifunza vizuri kwa usahihi na urahisi.

Mchungaji Rohho ameongeza kuwa kalenda ya KKKT hutengenezwa kwa kufuata na kwa kuzingatia kwa usahihi majira ya kanisa hivyo ni vema kila mkristo akaipata ili iweze kumsaidia kutambua majira na kujua Neno lililopo katika majira husika ya Kanisa.

Wakristo wote wanahimizwa kujijengea utaratibu wa kuwa na kalenda ya Kanisa na kuifuata kwa maana ndiyo inayotoa mwongozo kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na kwa waumini wake wote waliopo maeneo mbalimbali Nchini.

Kalenda za Kanisa zikitumiwa vizuri na hasa wakristo watu wazima wakizinunua na kuzitumia katika nyumba zao itasaidia sana na kuwa urithi mzuri kwa watoto na vijana wao kujua na kuelewa vizuri maneno ya Mungu katika majira yote ya mwaka wa Kanisa.

# Matukio ka



*Watenda kazi wa Ofisi Kuu na vituo vya Umoja KKKT wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kumalizika kwa mafunzo ya kuongeza u katika utendaji kazi.*



*Mhe. Askofu Renard K. Mtenji (Dayosisi ya Ulanga Kilombero) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajasiriamali wanaowezeshwa na KKKT.*



*Mkurugenzi wa wanawake na watoto KKKT, Bi. Faustina Nillan (wa kutoka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya semi unyumba iliyofanyika katika Mtaa wa Kilala Arusha.*




*Mwenyekiti wa Bodi ya LMC, Mhe. Askofu Dkt. Benson K. Bagonza (katikati) akiwa kwenye kikao na baadhi ya wajumbe wa Bodi hiyo.*



*Katibu Mkuu wa KKKT Bw. Brighton Killewa (wanne kutoka kushot akiwa na baadhi ya watenda kazi wa Ofisi Kuu na wanufaika wa T shufaa katika siku ya Maadhimisho ya Tiba Shufaa.*

# atika Picha



uwezo



tano
na ya



o)
iba



*Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Meru, Bw. Lazaro Urio (aliyevaa miwani) na Daudi Msseemmaa (aliyevaa shati za bluu), Mwakilishi wa ELCA Tanzania wakigawa chakula cha msaada kwa waathirika wa mafuriko.*



*Naibu Katibu Mkuu Misioini na Uinjilisti, Mch. Lazaro Rohho akizungumza jambo wakati wa Mkutano Mkuu wa vijana uliofanyika katika Dayosisi ya Morogoro hivi karibuni.*

## Msaada wahanga Mafuriko, Dayosisi ya Meru

Wakazi wa Samaria na Maroroni wamelishukuru KKKT na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani (ELCA) kwa kuwapa msaada wa chakula mara baada ya kupatwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha mwezi 4 mwaka huu na kuacha athari kubwa ya uharibifu wa mazao, mifugo, nyumba pamoja na miundo mbinu kwenye maeneo hayo ikiwa ni hasara ya zaidi ya Bilioni 4.9

Katibu Mkuu Dayosisi ya Meru, Bw. Lazaro Andrew Urio amesema kuwa Dayosisi hiyo ilichukua hatua za haraka kusaidia majimbo yaliyopatwa na mafuriko hayo ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha marafiki walio nje ya nchi ili kuweza kupata msaada wa haraka ambao utawawezesha waathirika kujikimu katika mahitaji yao.

Mwakilishi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani (ELCA) Bw. Daudi Mssemaa amesema kuwa msaada huo umetolewa ikiwa ni ishara ya upendo kwa wale wote waliofikwa na janga hilo na kusema kuwa Kanisa hilo litaendelea kushirikiana na KKKT ili kuhakisha waathirika wote wanapatiwa msaada wa haraka ili kuwakomboa katika mazingira magumu.

Naye mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Meru, Mhandisi Simon Mbaga, amesema kuwa Serekali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

KKKT imeendelea kuchukua hatua za haraka katika kuwasaidia waathirika wa mafuriko katika Dayosisi 5 ambazo ni Dayosisi ya Meru, Dayosisi ya Mwanga, Dayosisi ya Ulanga Kilombero, Dayosisi Ziwa Tanganyika na Dayosisi ya Kaskazini ikiwa ni njia mojawapo ya kuendelea kutoa huduma za Kiroho na Kimwili kwa watu wote.



*wanavikundi wa ujasiriamali wanaowezeshwa na KKKT kupitia Programu ya Maisha Endelevu na uwezeshaji wakionyesha mfano wa kazi wanazofanya kwa wageni wao kutoka Dodoma.*

# Bodi ya Ukaguzi KKKT

Bodi ya Ukaguzi ya Kanisa la kiinjili la kilutheri Tanzania, inafanya kazi kubwa ya kuhakiki taarifa mbalimbali za kifedha za Kanisa ambazo hutolewa na Dayosisi zake 26.

Bodi hiyo huendesha shughuli zake kwa kufanya vikao ambapo hupokea taarifa za kikaguzi za kifedha kutoka kwenye sharika na vituo mbalimbali vilivyopo chini ya Dayosisi na hivyo huzipitia kwa umakini na kisha kutoa maoni na mapendekezo juu ya taarifa hizo za ukaguzi ambazo hutumika kwa ajili ya kuijenga Dayosisi husika na Kanisa kwa ujumla.

Bodi hiyo ya ukaguzi ina wajumbe watano ambao wote uchaguliwa na mkutano Mkuu wa KKKT.

Bodi hiyo hufanya kazi kubwa katika Kanisa kwanza kwa kuhakikisha kuwa Mkaguzi Mkuu wa Kanisa anafanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa. Pili kuhakikisha taaluma ya kiukaguzi pamoja na misingi yake inalindwa vema na hayo hufanyika ili kurahisisha kazi za ukaguzi kufanyika kwa kuzingatia weledi.

Mbali na kukagua taarifa kutoka kwenye Dayosisi zote za KKKT, bodi pia hujadili taarifa mbalimbali za kiukaguzi kutoka kwenye vituo vya umoja na shughuli za umoja ambazo ni Shule ya viziwi Mwanga, Shule ya viziwi Njombe, Seminari ndogo ya kilutheri Morogoro, Kituo cha Elimu ya ushauri na utunzaji kichungaji kilichopo Moshi pamoja na Kituo cha matangazo Radio Sauti ya Injili.

Umuhimu wa kufanyika kwa ukaguzi katika Kanisa, unaelezwa kuwa ni jambo la msingi kwa ajili ya Kanisa na maendeleo ambapo Mwenyekiti wa Bodi ya ukaguzi ya KKKT, Bw. Gilbert Magande ameainisha kuwa ukaguzi husaidia kutunza nidhamu pamoja na kuboresha miongozo ya kifedha kupitia taratibu za kiukaguzi.

"Ukaguzi unafaida kubwa ya kutunza nidhamu, kuweka miongozo sahihi ya kiukaguzi, kuboresha utendaji na inaleta ari ya kiutendaji katika Kanisa" amesema Bw. Magande

Hayo yameungwa mkono pia na kaimu Mkaguzi Mkuu wa KKKT, Bw. Elisa E. Mhando kwa kusema kuwa katika vikao vya bodi, taarifa mbalimbali hupitiwa na ushauri utolewa kwa Kanisa ili kuweza kuboresha masuala yote ya utuzanji wa mambo ya fedha.

"ushauri unaotolewa katika vikao hivi mara baada ya kupitia taarifa mbalimbali, huelekezwa moja kwa moja kwenye Dayosisi pamoja na Halmashauri Kuu ya Kanisa ili kuboresha kazi ambazo Kanisa linafanya kwenye maeneo mbalimbali nchini" amesema Bw. Mhando.

Hata hivyo Bodi ya ukaguzi ya KKKT inayouwezo wa kutunga na kuboresha miongozo ambayo hufuatwa wakati wa taratibu za kiukaguzi zinapofanyika.

Bodi ya ukaguzi ya KKKT, hutoa ushauri kwa Halmashauri Kuu ya KKKT, kuhusiana na mambo mbalimbali yakiwemo masuala ya utunzaji wa mambo ya fedha, ajira, taratibu za kuwaadhibisha wakaguzi endapo wataenda kinyume na yanayohitajika, hayo yote ni katika kuboresha utanzaji na matumizi sahihi ya fedha za Kanisa.

> "Ukaguzi unafaida kubwa ya kutunza nidhamu, kuweka miongozo sahihi ya kiukaguzi, kuboresha utendaji na inaleta ari ya kiutendaji katika Kanisa"



*Baadhi ya wajumbe wa bodi ya Ukaguzi KKKT wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kumalizika kwa vikao vya bodi hiyo mjini Arusha..*




# Kanisa na watu wenye ulemavu

Na Peter Kayombo

Kumekuwa na muitikio mdogo wa watu wenye ulemavu kuhudhuria ibada katika makanisa yetu. Hii ni kutokana na dhana ya watu wenye ulemavu kuona wanatengwa na kutokujaliwa, kwa kupewa huduma stahiki kama vile kutokuwa na wakalimani wa lugha ya Alama kwa Viziwi, vyoo maalumu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, Biblia iliyo katika mfumo wa maandishi ya nukta nundu kwa watu wasioona nk. Hii husababisha watu wenye ulemavu kutopata au kupata kidogo sana haki yao ya kuabudu mara wawapo katika nyumba za Ibada.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lenye Taswira ya kuona ushirika wa watu wenye upendo, amani na furaha waliobarikiwa kiroho na kimwili, wenye matumaini ya kuurithi uzima wa milele kwa njia ya Yesu kristo na pia dhamira yake ni kuwafanya watu wote wamjue Yesu Kristo ili wawe na uzima tele kwa kuwahubiria habari njema kwa maneno na matendo, kwa kuzingatia Neno la Mungu kama ilivyo katika Biblia na Misingi ya mafundisho ya kilutheri kwa kuongozwa na katibaa ya KKKT.

Kanisa linasisitiza Upendo, kuwafanya watu wamjue Mungu, kuwasaidia wajane na watu wenye mahitaji maalumu au walemavu kwani wote tu wamoja katika Kristo Yesu na ndio upendo huo tunaouishi leo na hata milele.

KKKT ni jumuishi, linatangaza Injili na kuwakaribisha watu wote kujumuika katika ibada bila kujali ulemavu wao, kwetu sisi Ulemavu ni kazi ya uumbaji wa Mungu. Na ndio maana Yesu mara nyingi aliwarekebisha na kuwakemea wale waliotafsiri watu wenye ulemavu kwa mtazamo hasi.

Tunapoyachunguza maandiko matakatifu katika kitabu cha Yohana 9:1–3 tunaona pia kwamba ulemavu sio laana bali watu kuwa walemavu ni ili matendo ya Mungu yadhihirishwe ndani yao. Na ndio maana hata leo tunashuhudia watu wenye ulemavu mf. viziwi, wasioona, albino na watu wenye ulemavu wa viungo wanafanya kazi mbalimbali kama vile madaktari, walimu, maafisa ustawi wa jamii, wabunge, wakuu wa wilaya, wabunifu wa mavazi nk. hii yote ni kudhihirisha matendo makuu ya Mungu ndani yao kwamba pamoja na wao kuwa walemavu bado upo uwezekano wa wao kufanya mengi kupitia Yeye atutiaye nguvu.

Katika kuthibitisha dhana ya jumuishi inatekelezeka na Injili inafika kwa watu wote Kanisa limeanzisha mpango wa Mafunzo ya lugha ya Alama katika Mradi wake Uitwao "Njombe Mission To the Deaf" kwa kuwafundisha Watumishi wa Kanisa kama vile wachungaji, wainjilisti, mashemasi na walimu wa dini ili liweze kuwafikia watu wenye ulemavu wa kutosikia (Viziwi).

Kanisa limejikita kwenye kutoa hii Elimu kwani Ulemavu wa Uziwi ni ulemavu usio onekana kwa macho na unahitaji lugha maalumu ambayo ni lugha ya Alama katika mawasiliano ambayo ni tofauti na aina nyingine za ulemavu ambapo mtu mwenye ulemavu anatumia lugha ya kawaida katika mawasiliano na anasikia vyema.

Mpango huu ni endelevu na Kanisa linautekeleza katika shule ya Lugha ya Alama na wakalimani katika kituo chake cha Njombe Viziwi ili elimu hii iwafikie watu wengi ambao watasaidia watu wenye uziwi.

Kwa namna hiyo Kanisa litaweza kuzalisha wakalimani wa lugha ya Alama wengi ambao wataweza kuwasaidia watu wenye uziwi kupata huduma stahiki sehemu mbalimbali kama vile; hospitalini, mahakamani, polisi, Bank kwenye sehemu za ajira na hata kwenye shughuli zingine za kimaendeleo.

Ulemavu wa kutosikia (Uziwi) ni changamoto ambayo humfanya mtu

Inaendelea Uk. 14

# Vijana na Ajira

Na Joram Nkya

Zipo changamoto nyingi zinazowakumba vijana wa Tanzania na mojawapo ni suala la ajira, Jambo ambalo limekuwa mzigo na kilio kikubwa kwa vijana walio wengi wasomi na hata wale ambao hawajaenda shule.

Katika tafiti ndogo niliyokuwa nikifanya nimeweza kupata baadhi ya mambo ambayo vijana wa kitanzania wakiyajua na kuyafanya kama inavyotakiwa wanaweza kupiga hatua kimaisha na hivyo kuwakwamua katika suala zima la ukosefu wa ajira na matatizo ya kiuchumi.

Katika tafiti hiyo ndogo miaka kadhaa iliyopita nilibahatika kukutana na msichana mmoja msomi kutoka Sweden aliyekuja nchini kwa ajili ya kufanya utafiti na kuchukua taarifa kwa ajili ya andiko lake la shahada ya uzamivu (Phd).

Katika kujadiliana nae mambo kadhaa ya kisiasa na kiuchumi alinihakikishia kuwa bado Afrika suala la ukosefu wa ajira halipo kwa kiwango kikubwa kama lilivyo kwa nchi za ulaya na Marekani.

Nilivutiwa sana na maelezo hayo na nilitamani aendelee zaidi kuniambia hizo ajira katika bara la Afrika zipo wapi, bila hiana alinijuza wazi wazi kuwa zipo katika sekta ya kilimo na ujenzi.

Katika eneo kilimo aliniambia bado eneo kubwa la afrika na hasa Tanzania linafaa kwa kilimo na halijawahi kulimwa tangu kuwepo kwa misingi ya ulimwengu!

Maelezo hayo yalinifanya nifungue macho na masikio yangu na niligundua kuwa ni kweli kwamba; Kilimo kinauwezo wa kuajiri maelfu ya vijana wa nchi yetu na hata wasitoshe!

Vijana wengi wanaweza kujiajiri hata katika kilimo cha jembe la mkono na wakazalisha mali ya kutosha na kisha kuuza katika masoko ya ndani na hata nje.

Kilimo cha mbogamboga na matunda kama vijana watajikita vilivyo katika eneo hili ni dhahiri wanaweza kubadilisha maisha yao kuliko kukaa bila kufanya kazi yoyote.

Vijana wengi wanaona kilimo kama adhabu lakini ukweli ni kwamba ni katika sekta ya kilimo pekee ambapo vijana wana uhakika wa kupata ajira na chakula. Kwa baadhi ya vijana waliojielekeza katika eneo hili la kilimo na hata ufugaji wa kuku na sungura hilo limethibitika wazi kwao na kuwaondoa katika maisha ya utegemezi!

Katika kumalizia Makala hii nitoe wito kwa vijana wasio na ajira ya kwamba sekta ya kilimo ipo na ukiwekeza nguvu zako huko basi ule usemi kuwa jembe halimtupi mkulima kwako utatimia na kwa hivyo utaweza kujikwamua katika hali ya kiuchumi na kumaliza tatizo la utegemezi.

Mtaji wa kwanza kabisa kwa kijana ni nguvu zake za ujana! Nguvu hizi zikitumiwa vyema ni mtaji tosha za kujikwamua kiuchumi na kimaisha kwa ujumla.

Thubutu, uwe na ujasiri bila kukata tamaa kisha amua kuanza huku ukimtegemea Mungu na atasikia maombi yako na kubariki kazi za mikono yako na maisha yako hayakuwa kama yalivyokuwa hapo awali. Na inawezekana kabisa ukaanza peke yako lakini baadae kilimo kikawa kizuri na kikakuwezesha kuajiri na vijana wengine ambao bado hawana kazi.

Tukutane kwenye Makala nyingine ili tupate mwendelezo wa mazuri haya.



## Kanisa na watu wenye ulemavu

Inatoka Uk. 13

kushindwa kusikia sauti yoyote. Kwahiyo walemavu hawa wakiwa kanisani wanashindwa kusikia mahubiri na shughuli zote zinazoendelea ndani ya kanisa, yeye atakuwa anaona matendo tu lakini hasikii, washarika wengine wanapo furahi kwa nyimbo na mahubiri ya wachungaji yeye hasikii na wala kuelewa nini kinafundishwa anabaki tu amekaa na hii inapelekea washarika wengi wenye ulemavu huu kushindwa kuhudhuria kwenye ibada mbalimbali kwenye makanisa yetu kama vile ibada za jumapili, ibada za jumuiya na hata kwenye makongamano na shughuli mbali mbali za kikanisa kwani hawasikii nini kinachoendelea.

Hivyo ni vema katika Ibada kwenye makanisa kuwepo wakalimani wa lugha ya Alama ambao watakua wanawatafsiria Mahubiri ya Neno la Mungu pamoja na matangazo mbalimbali ya Kanisa ili watu wenye Uziwi nao waweze kulisikia na kulifurahia Neno la Mungu wakati wa Ibada.

"Tukiwatendea yaliyomema watu wenye Ulemavu basi tumemtendea Mungu" Peter S. Kayombo. Mratibu Misioni kwa Viziwi, KKKT.

# KKKT ilivyochukua hatua dhidi ya COVID 19



*Mkuu wa Kanisa Mhe. Askofu Dkt. Fredrick Shoo (watatu kutoka kulia) akikabidhi vifaa tiba kwa baadhi ya wafanyakazi wa Hospitali za kanisa nchini. Wakwanza kulia ni Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii wanawake na watoto, Mch. Rachel Axwesso akifuatiwa na Katibu Mkuu KKKT, Bw. Brighton Killewa.*

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limegawa vifaa tiba katika awamu mbili tofauti kwenye hospitali na vituo vyake vya Afya vilivyopo maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni kuendelea kuchukua tahadhari juu ya gonjwa la COVID–19 ikiwa litarudi tena.

Katika uzinduzi wa ugawaji vifaa tiba uliofanyika jijini Arusha, Mhe. Askofu Dkt. Fredrick Shoo ameeleza kuwa ugonjwa huo ulianzia Nchini China mwishoni mwa mwaka 2019 na baadae kusambaa kwa kasi katika maeneo mbalimbali wakati nchi nyingi Duniani zikiwa hazijafanya maandalizi ya kutosha katika kupambana na janga hilo.

Mhe. Askofu Dkt. Shoo amesema kuwa, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) liliweza kuchukua hatua stahiki katika kupambana na maabukizi ya virusi vya Corona ikiwemo ni kufanya maombi ili Mungu awasamehe watu wake pamoja na kuwaondolea janga hilo linaloitesa Dunia.

Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa Elimu kwa wakristo na watu wote juu ya maambukizi ya virusi vya Corona ili jamii iweze kufahamu namna sahihi ya kujikinga ili kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi hivyo.

Hatua nyingine pia zilizochukuliwa na KKKT ni pamoja na kupunguza safari mbalimbali za Kikanisa, kuondoa ratiba za mafundisho ya kipaimara, kupunguza idadi ya vikao na mengine mengi ili kudhibiti kasi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo.

Mhe. Askofu Dkt. shoo amesema kuwa ugonjwa huu ulileta madhara katika maeneo tofauti tofauti ikiwemo katika ngazi za kifamilia ambapo huko wapo waliowapoteza wapendwa wao ambao walikuwa tegemezi katika familia zao na kufanya familia kuwa katika hali ya uhitaji.

Wapo wengine pia waliopoteza ajira kwasababu shughuli nyingi za kuwaingizia watu vipato zilisimama na kusababisha mitaji kuanguka.

Ukatili wa kijinsia nao ulionekana kuwa moja ya madhara yaliyojitokeza katika kipindi ambacho watoto na wanafunzi wengi walikuwepo majumbani sababu ya kufungwa kwa shule na vyuo nchini. Mabinti wengi walijikuta katika adha hiyo kutoka kwa ndugu na jamaa kipindi wapo majumbani na kupelekea wengine kupata mimba, hali iliyosababisha migogoro ya kifamilia kutokea.

Zoezi la ugawaji wa vifaa tiba lilimalizika kwa maneno ya shukrani kutoka kwa Mkuu wa Kanisa Dkt Shoo ambapo aliwapongeza madaktari na wahudumu wote wa afya wa Hospitali za kanisa kwa namna walivyojitoa mstari wa mbele kwenye mapambano dhidi ya Corona ingawaje vifaa tiba havikutosha na ikabidi viongezwe ikiwa ni gharama zilizopo nje ya bajeti lakini bado madaktari na wauguzi hawakusita wala kukata tamaa katika kutumikia wito wao.

> Kwenye hitimisho Mhe. Askofu Dkt. Shoo amewashukuru pia watu wote na wadau "Act alliance" waliowezesha zoezi hilo kufanyika ikiwa ni juhudi za Kanisa kuunga Mkono Serekali dhidi ya mapambano ya COVID-19.

Kwenye hitimisho Mhe. Askofu Dkt. Shoo amewashukuru pia watu wote na wadau "Act alliance" waliowezesha zoezi hilo kufanyika ikiwa ni juhudi za Kanisa kuunga Mkono Serekali dhidi ya mapambano ya COVID–19.

Askofu Dkt. Shoo ametoa rai kuwa, watu wanapaswa kuendelea na maombi ili janga hili liweze kuisha duniani kote na amesisitiza pia, ni vyema na muhimu kuzingatia taratibu na maelekezo ya kiafya yanayolewa na wataalamu wa afya ili kuendelea kukaa salama.

Mkuu wa Kanisa Askofu Dkt. Shoo ameonya pia kuhusu vitendo vya ukatili kwenye familia na jamii na kutaka tabia hizo kuisha ili watu waishi kwa amani na upendo na pia amevitaka vyombo vya dola kuchukua hatua stahiki kwa wale wote wanaotekeleza vitendo hivyo.

# Uimarishaji wa utendajikazi, Kanisa na vituo vya Umoja

Katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Ofisi Kuu unaimarika na kukidhi Mpango Mkakati 2015–2025 Idara ya Mipango na Maendeleo ya Ofisi Kuu imeanzisha mradi uliodhaminiwa na Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) pamoja na Kanisa la Sweden ambao utasaidia kuwajengea uwezo wafanyakazi wa ofisi hiyo ili kufikia malengo yaliyowekwa na Kanisa.

Mradi huo utakaofanyika kwa muda wa miaka mitatu (2020–2022) umeanza kwanza kwa kuangalia namna ya Ofisi Kuu inaendesha shughuli zake na namna wafanyakazi wa Ofisi hiyo wanatekeleza wajibu wao na kama shughuli zao zinaakisi moja kwa moja katika kufikia malengo ya Kanisa.

Akizungumza kuhusu mradi huo Katibu Mkuu Bw. Brighton Killewa amewataka wafanyakazi wa ofisi hiyo kutoa ushirikiano wa kutosha kama kawaida yao ili mradi huo ufanyike vizuri na kuleta matokeo sahihi yatakayosaidia utendaji kazi wa Ofisi Kuu ya Kanisa.

Washauri wa mambo ya miradi na maendeleo Dkt. Godwin Kimaro na Dkt. Rogate Mshana wameshirikishwa katika mradi huo ili kuangalia kwa undani namna Ofisi Kuu inafanya kazi zake na kama itaweza kufikia malengo waliyojiwekea na pia wataendesha mafunzo kwa watendaji kazi wa ofisi hiyo ili kuwaongezea uwezo wa kiutendaji kazi kwenye sehemu zinazohitajika.

> "Programu hii imelenga kujua ni kwa namna gani Kanisa inaendesha shughuli zake na je ni wapi kunapaswa kuboreshwa kwa manufaa ya Kanisa"

Washauri hao walipata nafasi ya kupita kila Idara ili kujua ni kwa namna gani Idara hizo katika Ofisi Kuu zinachangia katika kufikia Dira ya Kanisa, na huko pia watatoa njia bora zitakazosaidia kuendesha shughuli za Idara hizo kwa ufanisi na wepesi zaidi zitakazosaidia kulijenga Kanisa.

"Programu hii imelenga kujua ni kwa namna gani Kanisa inaendesha shughuli zake na je ni wapi kunapaswa kuboreshwa kwa manufaa ya Kanisa" amesema Dkt. Godwin Kimaro.

Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo Bw. Simon Daffi ambaye ndiye msimamizi wa mradi huo amesema mradi huo umedhamiria kuwawezesha wafanyakazi wa Ofisi Kuu kufanya kazi zao kwa weledi ili kufanikisha malengo ya KKKT.

"tunafanya zoezi hili la kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa Ofisi Kuu ili kuwawezesha kufikia malengo yaliyowekwa na Kanisa" amesema Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo Bw. Daffi.

Mradi huo umeanzia Ofisi Kuu ya Kanisa na baadae utapita katika vituo vitano vya Umoja ambavyo ni Radio Sauti ya Injili, Shule ya viziwi Mwanga, Shule ya viziwi Njombe, Seminari ya kilutheri Morogoro, pamoja na kutembelea Kituo cha Elimu ya Ushauri na Utunzaji Kichungaji kilichopo Moshi, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wafanyakazi wa ofisi hizo.



*Menejimenti ya Ofisi Kuu KKKT, wakifuatilia maelekezo ya mradi kutoka kwa Mshauri wa Miradi na Maendeleo, Dkt. Rogate Mshana.*

# Marehemu Seth Ndesanjo Kitange



*Marehemu Seth Ndesanjo Kitange.*

Katika historia za watu waliofanya kazi Kanisani na kutumika katika nafasi mbalimbali kwa kusudu la kumtumikia Mungu na kulijenga Kanisa basi Mzee Seth Ndesanjo Kitange ni miongoni mwao ambaye alilitumikia Kanisa kwa muda wa miaka 50.

Mzee Seth alikuwa ni mwenye ukarimu, mnyenyekevu, na mchapakazi na kwa ujuzi wake aliweza kulitumikia Kanisa akiwa ndani na hata nje ya nchi.

Mzee Seth alifanya mambo mengi wakati wa uhai wake ambapo alitumika kwa moyo wote bila kujali changmoto mbalimbali zilizomzunguka ama kutokea wakati afanyapo kazi zake.

Alipenda kushirikiana na wengine ili kuhakikisha kazi ya Mungu inasonga mbele. Alikuwa mkarimu mwenye kupenda haki na kuitoa pia pasipo kujali umri kwa wakubwa na wadogo.

Sethi Ndesanjo Kitange alikuwa Baba wa watoto wawili na mke mmoja, alizaliwa tarehe 22 Julai 1938 katika kijiji cha Mowo Old Moshi–Kilimanjaro akiwa ni mtoto wa Mchungaji Ndesanjo Kitange na Mama Elisia Masao na alibatizwa tarehe 25 Septemba 1938 katika usharika wa Mowo.

Safari yake ya Elimu ilianza katika shule ya msingi Shia ambapo alisoma na kumaliza elimu hiyo ya awali mwaka 1948–1953. Baadae aliendelea na elimu ya juu katika chuo cha Ualimu Marangu mwaka 1954–1957 na baada ya muda mfupi aliendelea na masomo yake katika chuo kikuu cha Nairobi mwaka 1958–1962. Na ulipofika mwaka 1965–1966 Seth aliamua kusomea mambo ya habari huko nchini Kenya kwa kusoma diploma ya uandishi wa habari katika chuo kikuu cha uandishi wa habari Nairobi.

Safari hiyo ya elimu haikuishia Tanzania na Kenya pekee bali aliweza kuvuka mipaka kutoka nje ya Bara la Afrika na kwenda hadi Amerika ambapo huko aliweza kusoma shahada ya mawasiliano katika chuo cha Bethany Virginia mwaka 1979–1982 na alihitimu masomo yake huko Albana Marekani kwa kusoma shahada ya Uzamili ya uandishi wa habari (masters of science Journalism) mwaka 1981–1982.

Mzee Seth alianza kazi rasmi kwa kufundisha katika shule ya msingi kidia mnamo mwaka 1958–1959 na baadae kuhamia kufundisha shule ya msingi Shia, shule aliyowahi kusoma akiwa mtoto. Na katika kipindi cha mwaka 1961–1964 alikuwa akifundisha katika chuo cha Biblia Mwika Kilimanjaro.

Baada ya kufundisha kwa muda Seth aliamua kujikita katika maswala ya habari na kwasababu ya utendaji wake wa kazi ambao ni wa ufanisi na kutukuka kulimpa nafasi ya kuwa mwandishi wa habari katika gazeti la "Target" na Lengo ambalo lilikuwa likichapishwa katika Nchi ya Kenya (Nairobi) na Tanzania (Dar es Salam) katika miaka ya 1964–1970 gazeti ambalo lilimilikiwa na Kanisa.

Seth alikuwa mtu wa kazi aliyezingatia weledi wakati wote, hivyo kulimpa nafasi pia katika Gazeti la "Daily Nation" la Kenya ambapo aliajiriwa na kufanya kazi akiwa ni Mhariri wa gazeti hilo katika miaka ya 1971–1976 na kwa juhudi zake katika tasnia ya habari alipandishwa cheo na kuwa Mhariri Mkuu wa Gazeti la "Target" na Lengo 1977–1978 yaliyochapwa na kuuzwa katika nchi mbili tofauti (Kenya na Tanzania).

Aliendelea kufanya kazi hiyo ya uandishi wa habari akiwa Mhariri na mshauri wa magazeti mbalimbali yakiwemo gazeti la Mwananchi, gazeti la Umoja (Dayosisi ya Kaskazini) katika miaka 1979–1994 wakati huo huo katika miaka ya 1988–1993 alikuwa Katibu Idara ya mawasiliano Dayosisi ya Kaskazini. Seth alifanya kazi pia katika Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (Lutheran World Federation) mwaka 1995 kama Mshauri wa mambo ya mawasiliano.

Kama alivyokuwa akifanya kazi nje ya nchi kwa kuzingatia weledi na kujituma hivyo hivyo ndivyo alivyofanya kazi zake ndani ya Nchi hasa katika Dayosisi yake ambapo alikuwa mchapa kazi asiyekuwa na kushindwa mwenye uthubutu wa kufanya yaliyo mazuri kwa watu wote na kwa namna hiyo alipata na nafasi ya kufanya kazi kama Katibu Mkuu wa Dayosisi Kaskazini katika miaka ya 1994–2003.

Kanisa lilitambua na kuona uchapakazi wake na hivyo mnamo 2004–2006 alipata nafasi ya kuwa Katibu Mwandishi wa Kanisa na kuitumikia vema kwa kadiri alivyoweza na ni katika kipindi hicho hicho alikuwa pia Mwenyekiti wa Radio Sauti ya Injili.

Mchango wake mkubwa ulionekana pia pale alipokuwa Msimamizi Mkuu katika kituo cha uchapishaji moshi (Moshi Lutheran Printing Press) ambapo alifanya kazi kwa muda usiopungua masaa 12–15 kwa siku.

Yapo mengi aliyoyafanya Sethi Ndesanjo Kitange na haya ni katika yale makubwa machache aliyoyafanya, kwa mengine ambayo hayapo humu basi uungana nasi katika Makala yajayo.

2004–2006 Katibu Mwandishi wa Kanisa (KKKT) na Katibu Idara ya Mawasiliano wa Dayosisi ya Kaskazini na Mwenyekiti Radio Sauti ya Injili

2007–2015 Katibu Idara ya Mawasiliano na Meneja Moshi 'Printing Press' 1958–1959 shule ya msingi kidia, alifundisha

1960–1961 shule ya msingi shia 1961–1964 mkufunzi chuo cha Biblia mwika 1964–1970 Mwandishi wa Target na Lengo Dsm na Nairobi, Gazeti la Kanisa 1971–1976 Mhariri Gazeti la DailyNation Kenya 1977–1978 Mhariri Mkuu Target na Lengo 1979–1980 Mshauri Gazeti la Mwananchi na Afro lead

Inaendelea Uk. 18

# Vikundi Ulanga Kilombero washukuru Kanisa

Baadhi ya vikundi vya ujasiriamali vilivyopo chini ya Dayosisi ya Ulanga Kilombero (Morogoro) walishukuru Kanisa na ofisi kuu ya KKKT kwa namna ambavyo limekuwa likiwasaidia katika kupiga hatua kimaisha kupitia Programu ya Maisha Endelevu na Uwezeshwaji.

Vikundi hivyo vinavyojishughulisha na ufugaji, kilimo, utengenezaji batiki na mengine mengi kutoka kwenye Dayosisi ya Ulanga Kilombero kwa pamoja vimesema kuwa uwezeshwaji uliofanywa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ndio ambao umewasaidia kuwaongezea kipato hivyo kuwa na uwezo wa kumudu maisha yao ya kila siku.

Vikundi wenyeji kutoka Dayosisi hiyo (Ulanga Kilombero) Kilimo kwanza na wapendanao vikipokea ugeni wa vikundi vinne kutoka Kondoa Dodoma ambavyo ni Pambana na hali yako, Huruma, Safina pamoja na Mana, walioenda kujifunza kutoka kwenye vikundi vya Dayosisi hiyo wametoa ushirikiano mzuri hasa katika kuwa kuwaonesha vikundi kutoka Dodoma namna wamefanikiwa katika utekelezaji wa shughuli zao lengo likiwa ni kubadilishana elimu na uzoefu katika shughuli za ujasiriamali.

KKKT katika kutimiza Taswira yake kuona ushirika wa watu wenye upendo, amani na furaha waliobarikiwa kiroho na kimwili, wenye matumaini ya kurithi uzima wa milele kwa njia ya Yesu kristo ndio jambo ambalo Idara ya Mipango na Maendeleo kupitia programu ya maisha endelevu na uwezeshaji inatekeleza katika Mikoa mbalimbali kupitia vikundi vilivyoundwa na wanajamii bila kujali dini, kabila ama itikadi yoyote tayari kwa kupokea elimu na uwezeshwaji ili kuwa na maisha mazuri yaliyoendelevu.

Ifahamike vizuri kuwa hii ni njia mojawapo pia ya kutimiza ile dhamira ya KKKT ambayo ni kuwafanya watu wote wamjue Yesu Kristo ili wawe na uzima tele kwa kuwahubiria habari njema kwa maneno na vitendo, kwa kuzingatia Neno la Mungu kama ilivyo katika Biblia na Misingi ya mafundisho ya kilutheri kwa kuongozwa na katiba ya KKKT.

Hivyo mbali na kuwahubiria kwa maneno kuhusu habari njema za Yesu pia kwa vitendo Kanisa linaendelea na kazi hiyo ili wale wote waliosikia habari za Kristo Yesu waendelee kuona kwa matendo namna Kanisa linawagusa kwa njia mbalimbali ili kuwapa watu maisha yaliyo mazuri waweze kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Baadhi ya Mikoa ambayo kwa sasa inaguswa na programu hii ya Maisha Endelevu na Uwezeshaji ni Njombe, Mbeya, Iringa, Dodoma, Morogoro nk. ikiwa ni juhudi za kuwakwamua watu kutoka katika kipato cha chini cha maisha na kuwasogeza mahali ambapo wataweza kumudu mahitaji yao kila siku na yamkini kusaidia na wale wanaowazunguka mara wanapohitaji msaada kutoka kwao ikiwa ni dhumuni la kuwa na jamii yenye maisha endelevu.

Programu hii inayoratibishwa na Mratibu Bi. Patricia Mchome kutoka Ofisi ya KKKT (Arusha) imejikita katika kuisadia jamii msaada wa kielimu na rasilimali vitu ili wao waweze kuvitumia kwa ufasaha na kuwaletea matokeo chanya katika kumudu maisha yao ya kila siku.

Baadhi ya vikundi vilivyowezeshwa na programu hiyo, vimeweza kujimuudu na kusonga mbele zaidi na hata kutengeneza miradi yao kama vile mashine za kukoboa na kusaga nk. ikiwa ni katika kuboresha hali yao kiuchumi na kupiga hatua mbele ili kujiongezea namna ya upatikanaji wa kipato katika Kundi kwa faida ya wanakikundi wote.

Programuu ya Maisha endelevu na uwezeshaji imekusudia kufikia wengi na inaendelea kutoa elimu na kuziwezesha jamii katika nyanja mbalimbali ili wawe na maisha mazuri na endelevu sasa na hata baadae.

# Marehemu Seth Ndesanjo

Inatoka Uk. 17

1982–88 Mhariri Africa news services Amerika

1988–94 Mhariri wa Gazeti la Umoja Dayosisi ya Kaskazini

1995 Mshauri wa Mawasiliano LWF Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani

1988–93 Katibu Idara ya mawasiliano Dayosisi ya kaskazini

1994–2003 Katibu Mkuu Dayosisi ya Kaskazini

2004–2006 Katibu Mwandishi wa Kanisa (KKKT) + Katibu Idara ya Mawasiliano wa Dayosisi ya Kaskazini na M/kt Radio Sauti ya Injili

2007–2015 Katibu Idara ya Mawasiliano + Manager Moshi Printing Press

Seth alikuwa mnyenyekevu mwenye kupenda kazi yake na aliyejituma kufanya kazi katika mazingira yoyote bila kujali changamoto zozote zilizomkabili.

Seth alifanya kazi kwa masaa yasiopugua 12–15 kwa siku

Hata kipindi cha kuugua bado aliendelea kufanya kazi akiwa kitandani

Aliwapenda watu wa rika zote na kutoa haki kwa mkubwa na hata mdogo

Mwandishi wa Maandiko mbalimbali: New millennium books Uamsho na karama Kanisa na makanisa Journal to freedom Vumipugoa Tumsifu Bwana (kitabu cha ibada ya watoto kilichotumika kwenye Dayosisi 5 za KKKT ukanda wa kaskazini)

Diakonia na vingine vingi

Seth Ndesanjo Kitange

Seth alianza elimu yake kwenye shule ya msingi Shia Darasa la kwanza hadi la nane (1948–1953). Alimaliza elimu yake ya juu katika chuo cha Ualimu marangu (1954–1957) na alisoma chuo Kikuu cha Nairobi (1958–1962).

1965–1966 diploma ya uandishi wa habari chuo kikuu cha uandishi wa habari Nairobi Kenya.

1979– 1981 chuo cha Bethani Vejinia Amerika shahada ya mawasiliano

1981–1982 shahada ya uzamili ya uandishi wa habari (masters of science Journalism) chuo kikuu cha ienenozi albana Amerika

alifikwa na umauti siku ya 15/10/2020 kutokana na ugonjwa wa Kisukari na Shinikizo la Damu akiwa na umri wa miaka 82. Sethi alilitumikia Kanisa kwa muda wa miaka 50.

# Mkutano Mkuu Vijana KKKT

Vijana wa KKKT wametakiwa kuwa mstari wa mbele katika kulijenga Kanisa bila kusahau kuchukua hatua za msingi za kujituma katika kazi na shughuli mbalimbali ili waweze kujikimu kimaisha na kuwa msaada kwa jamii inayowazunguka.

Hayo yamezungumzwa katika Mkutano Mkuu wa Vijana ulioandaliwa na Dawati la Vijana KKKT linaloongozwa na Mchungaji Frank Mexon Mng'ong'o ambapo umewakutanisha viongozi na wawakilishi wa vijana kutoka Dayosisi zote 26 za KKKT na maeneo mawili ya Misioni ambapo katika mkutano huo mambo muhimu yahusuyo vijana na namna ya kuwajenga vijana wa KKKT ili wawe chachu ya maendeleo katika Kanisa na maeneo waliyopo yalizungumzwa kwa kina.

Mkutano huo ulifunguliwa na Mhe. Askofu wa Dayosisi ya Morogoro Paul Jacob Mameyo ambaye alisema kuwa, misingi ya kilutheri ni vema ikazingatiwa ili kuendeleza kulijenga Kanisa kama watangulizi walivyofanya maana pasipo kufanyika hivyo itakuwa ni ngumu kuwa na Kanisa lenye Umoja na litakalo dumu.

Mhe. Askofu Mameyo amewataka viongozi wa vijana kushirikiana kwa karibu na vijana wanaowaongoza ili kuwasaidia katika changamoto mbalimbali wanazokumbuna nazo ili kuweza kuwa na Kanisa lenye vijana waliojengewa misingi mizuri na ambao watakuwa na umoja.

Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT, Mchungaji Lazaro Rohho ambaye naye alishirikika katika mkutano huo ulioandaliwa na Dawati la Vijana lililo katika Idara yake alisema kuwa ni vema vijana wakazingatia uadilifu jambo ambalo litawajengea picha nzuri juu ya maisha yao na kuwataka kutumia nguvu zao katika kutenda mambo yanayofaa.

Naibu Katibu Mkuu, Mchungaji Rohho amesema kuwa pamoja na kuhakikisha kuwa vijana wanajengewa misingi mizuri ya Kikanisa lakini ni vema watoto wadogo wasisahauliwe ili elimu ya Kikristo izidi kuwa imara ndani yao na watakapokuwa vijana waendelee kulijenga Kanisa kwa nguvu zao zote.

Mratibu wa Vijana KKKT, Mchungaji Frank Mng'ong'o pia ameukumbusha Mkutano huo kuwa kuongoza vijana katika nyakati hizi kunahitaji Hekima ya kipekee kutoka kwa Mungu ambapo mabadiliko ni mengi na walengwa wakubwa ni vijana hivyo viongozi wanapaswa kuwa mstari wa mbele ili kuwasaidia vijana katika changamoto wanazokutana nazo katika maisha yao ya kila siku.

Naye Mwenyekiti wa Mkutano huo Julian Kagambo akizungumza wakati wa Mkutano huo amesema umoja na kuvumiliana ndio jambo la msingi katika kuongoza vijana hivyo ni vema hayo yakazingatiwa ili kuendelea kuwajenga vijana wa KKKT waweze kutoa mchango wao mkubwa kupitia karama walizonazo.

Mkutano huo ulioambatana na warsha ya siku moja, uliwaasa viongozi hao kuwa mfano kwa vijana wanaowaongoza na pia kuwahamasisha vijana kutumia vizuri fursa zilizopo mbele yao za kiuchumi na kibiashara na kuwa makini katika matumizi ya mitandao ya kijamii ili iwaletee faida.

Wawezeshaji katika warsha hiyo Bi. Neng'ida Johhannes Mkurugenzi Mtendaji wa Upendo Media na Bw. Ibrahimu Mwangalaba Mkurugenzi Mtendaji Maendeleo Banki wametaka viongozi hao wa vijana kuchangamkia fursa na waweze kutumia mitandao ya kijamii kufanya shughuli za msingi ambazo zitawaingizia kipato cha kuweza kujikimu katika maisha.

Wawezeshaji hao Bi. Neng'ida na Bw. Mwangalaba waliwaambia vijana kuwa Upendo Media pamoja na Maendeleo Bank zipo kwa ajili yao ikiwa wataweka juhudi na kuwakikishia kuwa watakuwa tayari kuwasaidia katika hali yoyote ikiwa watakuwa wamejipanga vizuri.


Katika kuhitimisha Mkutano huo Askofu Mlezi wa Vijana wa KKKT Mhe. Dkt. Emmanuel Makala amewataka viongozi hao wa vijana kuhakikisha wanayafanyia kazi mambo yote waliyokubaliana katika mkutano huo na kutumia vizuri fursa zilizotolewa na Upendo Media na Maendeleo Bank ili waweze kufaidika na kuendeleza kulijenga Kanisa.



*Viongozi wa Vijana wakifuatilia jambo wakati wa Mkutano Mkuu wa Vijana KKKT uliofanyika katika Dayosisi ya Morogoro.*

# Kalenda KKKT, Kitabu cha Nyumba kwa Nyumba vya mwaka 2021 vinapatikana kwenye maduka ya KKKT




Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA